

EDENI YA SHETANI

 Hebu tuinamishe... Mungu mpenzi, tunakushukuru kwa nafasi hii nzuri sana ya kuja tena katika Jina la Bwana Yesu, kumkabili adui wetu; adui Wako huku kwenye uwanja wa mapambano tukiwa na Neno ili kumfukuzia mbali toka mionganini mwa watu Wako, ili wawewe kuona usiku huu, Bwana, Nuru ya Injili. Ninaomba utupake mafuta macho yetu kwa dawa ya kujiapaka macho ili yafumbuliwe kwenye kweli; ili tuweze kuondoka hapa, tukisema miyoni mwetu, "Je! miyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani." Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Watie nguvu waliovunjika miyo. Iinue mikono iliyo minyonge ambayo wakati mmoja ililemewa. Hebu na tukutazamie kuja kwa Bwana Yesu, ambako tunaamini kunakaribia. Twaomba hili katika Jina la Yesu. Amina. Ketini.

Nitajaribu kufupisha usiku wa leo, kwa sababu najua wengi wamekuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi kwa ibada; au wamebakii humu, baadhi yenu, na yawapasa murudi mpate labda njia ya kurudi, na nawashukuru. Asubuhi hii nilitaka kumsikiliza Ndugu Neville, mimi mwenyewe. Nimemsikiliza mara nyingi, na sijamsikiliza hata wakati mmoja, bila kumpenda, lakini asubuhi hii—ujumbe ule uliokuja kwa wakati uliofaa—najua mimi nilikuwa na uongozi wa Bwana kuusikiliza asubuhi hii. Mzuri sana. Na naona kwa nini ninyi watu mmapenda kuja kumsikiliza, pia. Na ye ye siku zote atawafaa, nina hakika, kumsikiliza.

Nilikuwa ninajaribu kufanya baadhi ya mahojiano yangu leo; asubuhi hii, na alasiri ya leo. Bado nimebakiza watu wengi, wengi sana.

Na kama ninavyoamini ilikuwa Yethro aliyemwambia Musa wakati mmoja, akasema, "Mzigo wako ni mkubwa sana." Kwa hivyo, tunao ndugu wengi sana hapa kwa ajili ya matatizo yenu, na kila moja yayo ni halisi, na ni mambo mazuri yanayopaswa kushughulikiwa. Na ningewashauri mumwendee mchungaji wetu au ndugu Mann, na wahudumu wengine wa imani yetu hapa —mwawenza kuwaendea. Wangewaambia sawa kabisa jambo la kutenda. Baadhi ya watu, watoto wao; kuoana, au mambo yasiyo mema. Watu hawa wanawenza kuwasaidia vile vile kama mtu mwingine ye yote, kwa sababu ni watumishi wa Kristo. Waendeeni, na nina hakika watawapeni msaada mnaohitaji. Siwezi kuwafikia wote. Wapo wengi sana kila mahali uendapo. Wanaendelea kuongezeka zaidi na zaidi, unaona; nawe unataka kumwendea kila mmoja wao, lakini huwezi kutenda hivyo. Lakini ninaomba wakati wote kwamba Mungu, kwa namna fulani, ataliweka lote sawa kwa ajili yako.

Sasa, usiku wa leo, tunataka kuyaendea Maandiko, na kusoma sehemu ya Maandiko kutoka Mwanzo, sura ya 3; na kurejea tu nyuma kidogo kwenye baadhi ya mambo ambayo tumekuwa tukiyazungumzia katika nyakati zilizopita, na kuona kwamba Bwana Yesu atatupa cha zaidi kidogo tupate kujua tutakapoondoka. Naomba kwamba yeche atafanya hivyo.

“Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! hivi ndivyo alivyo sema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?

Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula;

Lakini matunda ya miti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.

Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa;

Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya miti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.

Mwanamke alipoona ya kuwa ule miti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni miti wa kutamanika kwa maarifa, alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.

Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanya nguo.”

Bwana na aongezee baraka Zake katika kulisoma Neno Lake.

Sasa, ningependa kuchukua kifungu usiku huu kutoka katika hayo, na kukiita; *Edeni ya Shetani* – ni jambo dogo la kijinga sana kusema, “Kwenye Edeni ya Shetani.” Kwa namna fulani inalingana na usiku wa Jumapili iliyopita, ninaamini, nilipowazungumzieni hapa kuhusu *Chujio la Mtu Mwenye Busara, na Ladha ya Mtu Mtakatifu*. Na wakati mwengine hii misemo ya kijinga hutufikisha kwenye kitu fulani, na kutufanya tujifunze na hukufanya kulisoma Neno. Hilo ndilo ambalo ninataka kusanyiko langu kufanya. “*Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*” Kwa hiyo soma Neno; lisome kirefu. Basi lisome kirefu kwa macho ya Mungu ili kukuelewesha akili yako jinsi ambavyo tunapaswa kuishi katika wakati huu wa sasa.

Sasa, kuja usiku wa leo tu kuzungumza nanyi kusema, “Vema, ningeweza kufanya hili au lile.” Ningependa kunena na watu, kiasi ambacho ningependa hata kwenda nyumbani na kila mmoja wenu usiku wa leo. Mungu ajua hiyo ni kweli. Ningependa kwenda nyumbani na kila mmoja wenu, na

kula chakula cha asubuhi pamoja nanyi asubuhi, na kwenda kuwinda kindi pamoja nanyi kesho alasiri, mwaona. Ningependa kufanya hilo, bali siwezi kufanya hivyo. Na ningependa kwenda nyumbani na kuketi tu na kuzungumza nanyi; kuketi kwenye sebule baada ya ibada, na kuzungumza nanyi kwa muda kidogo na kuzungumza nanyi kuhusu ufanisi wa maisha yenu na kuhusu Mungu. Ningependa kufanya hilo. Wanaume na wanawake mliopo hapa; Mungu ajua ningependa kufanya hilo, lakini siwezi kulifanya. Kuna mvuto na uchovu mwangi wa akili. Na katika wakati huu wa wasiwasi ambao tunaishi—na mimi mwenyewe ni mtu mwenye wasiwasi.

Leo, nimeamua kitu fulani. Inanipasa kukifanya, na kesho kiko mamilioni ya maili mbali nami; na kitu fulani kimeingilia na kufanya hili na lile. Unao wakati mgumu kujaribu kuweka mawazo yako sawasawa. Lakini mafanikio yangu muhimu ni kulihubiria Kanisa Injili, na kufanya yote niwezayo kumletea heshima Yesu Kristo katika siku hii nikiwa hapa duniani, na Muda wangu uliobakia duniani.

Ninakuja kuwaambia kitu ambacho kitawasaki—kitu ambacho nimejifunza baada ya kwenda nyumbani asubuhi hii: Je! ningeweza kusema nini usiku wa leo, Bwana, ambacho kingewasaki watu wale. Nilipokuwa ninasikiliza ule ujumbe mkuu asubuhi hii juu ya... Ndugu Neville aliotuletea, kuhusu... Nilifikiria ulikuwa wa ajabu sana, jinsi alivyosema hapo, “Daktari ataugundua ugonjwa, lakini mtu yule anayekuja na kikarai kilichojaa sindano—hudunga sindano;” kwa hiyo nilifikiria kwamba huo ulikuwa msemo mdogo unaovutia, nilifikiria kuhusu hilo—dawa ile ya sindano, baada ya ugonjwa kutambulika. Na kwa hiyo, hilo ni jambo zuri sana.

Nilitaka kuongea nanyi kitu fulani; kuwaleteeni kitu kuwamulikieni ahadi ya Mungu kwa wakati huu, mnaona. Kitusi kitu ambacho mtu mwininge alikuwa nacho katika wakati uliopita, lakini kitu... na mambo hayo ni sawa; sote tunayataja mambo hayo. Lakini nilifikiria ningejaribu kuwaleteeni jambo fulani kwenye mawazo yenu kwa Maandiko haya niliyoandika hapa, ambayo yangewapa mwanga kujua—kukufanya askari bora zaidi katika sehemu mnayopiganiana sasa, kujifunza mbinu za adui ili muweze kuziba kila kitu kabla hajawafikieni, mnaona. Hicho ndicho kitu muhimu: ni kujifunza kujikinga na makonde kiasi unavyoweza.

Sasa, hebu tuangalie, sasa, kwa hii iliyo kuu... kwa dakika chache—siku hii kuu ya dhambi ambamo tunaishi. Siamini kwamba kuliwahi kuwa na siku ambayo niliwahi kusoma katika historia—kumekuwepo na wakati mkubwa zaidi wa mateso wakati ambapo wana wa Mungu walivawa kila upande, lakini kuuona udanganyifu wa adui, kamwe hatujawahi kuwa na wakati kama huu tunaoishi sasa, ni wakati wa ujanja sana, udanganyifu kuliko wakati wo wote. Na ninapoonaa hilo,

huniletea hili kwamba Mkristo anapaswa kuwa mwangalifu zaidi siku ya leo, kuliko alivyowahi kuwa katika wakati mwingine wo wote.

Sasa, huko nyuma katika siku za mateso ya Rumi kwa kanisa—Mkristo akifanya kosa, alikwenda kwenye uwanja wa michezo, na alilishwa simba au kitu kama hicho, wakati walipompata kuwa Mkristo kwa ajili ya ushuhuda wake. Lakini nafsi yake iliockolewa, kwa sababu alikuwa msafi, mwamini asiyeghoshiwa katika Mungu na kwa furaha alitia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake wakati mishipa yake ilipoachilia, au matundu katika mwili wake, yalipoachilia na damu ikatiririka, angepaza sauti, kwa imani ya kweli na ya uaminifu, na kusema, “Pokea roho yangu, Bwana Yesu.”

Lakini sasa, ujanja wa ibilisi sasa, huwafanya watu waamini kwamba wao ni Wakristo ambapo sio. Jambo ndilo hilo hapo. Si lazima kutia muhuri... Ni siku yenye hila sana kuliko vile ingelikuwa ambapo ilikulazimu kutia muhuri uhai wako kwa ushuhuda wako. Ibilisi ametega kila mtego wa ujanja unaoweza ku...ye ye ni mdanganyifu.

Na Yesu alituambia katika Mathayo 24 jinsi ambavyo siku hii ingekuwa ambamo tunaishi—siku ya udanganyifu sana iliyowahi kuwepo; karibu sana kwamba ingewadanganya wale walioteuliwa na Mungu kama ingewezekana kwa ye ye kudanganya.

Sasa, hebu na tulinganishe baadhi ya Maandiko, (au matabiri) yalionenwa katika Biblia kwa siku ya leo, na kuyalinganisha na siku ya leo tunayoishi. Katika II Timetheo sura ya 3, tulijifunza hili: Kwamba nabii alisema kwamba itakuwa katika siku hizi, kwamba watu wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu.

Linganisha hilo sasa, kwa muda tu. Hatuta... tutalielezea tu kifupi, kwa sababu hatuna muda huo wa kulipitia lote kama ambavyo ingetupasa kulichukua, lakini kuliweka tu wazi sasa, ili uweze kuona wakati utakapofika nyumbani na kujifunza hilo. Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, (wasiojizua) na wasiopenda mema. Sasa, Roho alinena waziwazi kwamba mambo haya yangekuwepo katika siku za usoni. Yaani siku hizi—unabii ukinena kwa habari zake.

Sasa, twasoma, pia, katika Ufunuo 14, Ufunuo 3:14 hasa, (Wakati wa Kanisa la Laodikia) kwamba ambavyo kanisa lingekuwa katika siku hii ya mwisho. Na ingekuwa... Unasema lingekaa kama mjane na asiwe na haja ya kitu. Lilikuwa tajiri, na limejitajirisha katika mali, na halijui kwamba wao walikuwa ni maskini, wenye mashaka, wanyonge, vipofu, na uchi, na hawakujua.

Sasa, kumbuka, Yeye ananena na kanisa la wakati huu—wanyonge, vipofu, uchi, na hawajui. Kifungu hicho cha mwisho—neno hilo la mwisho ndilo linalolifanya la kushangaza sana. Wanafikiria kwamba wamejazwa vizuri na Roho. Wote wako tayari... Wakati wa Kanisa la Laodikia ni Wakati wa Kanisa la Kipentekoste, kwa sababu ndio Wakati wa mwisho wa Kanisa.

Luther alikuwa na ujumbe wake. Wesley alikuwa na ujumbe wake, na Pentekoste walikuwa na ujumbe wao. Pia, ulisema, “Kwamba kwa sababu una uvuguvugu, si moto wala baridi”—mishtuko ya kimwili, ujuzi wa Injili wa akili, “Kwa sababu” Yeye alisema, “uko jinsi hiyo, nitakutapika utoke katika kinywa Changu.” Kwa maneno mengine, ilimtia kichefuchefu kuliona kanisa katika hali hiyo. Na kumbuka, walimtapika, na Yeye alikuwa nje ya kanisa akijaribu kuingia ndani tena katika Wakati ule mbaya sana wa Kanisa la Laodikia.

Mungu wa ulimwengu huu, leo—mtu yule anayeabudiwa wa dunia hii leo ni Shetani, nao watu hawajui wanamwabudu Shetani. Lakini ni Shetani anayejifanya mwenyewe kanisa, unaona—kama kanisa. Wanamwabudu Shetani, wakifikiria kwamba wanamwabudu Mungu kwa kupitia kanisa, lakini hivyo ndivyo Shetani amelifanya.

Loo! Unasema, “Lakini hebu ngoja kidogo; sisi tunahubiri Neno.” Angalia nyuma hapa kwenye somo langu, usiku wa leo. Shetani ndiye ambaye alimhubiri Hawa Neno kwanza. Mungu alisema, unaona. Ni kule kukosa kuelewa na sehemu hiyo ya Andiko ambalo linahusu wakati huo. Atakuachilia ujue yote yale Yesu aliyotenda yalikuwa sawa kabisa. Atakuachilia ujue yote yale Musa aliyotenda yalikuwa sawa kabisa. Lakini unapochukua ahadi ambazo wamenena kwa ajili ya siku hii; basi hizo zililhusika na wakati mwingine. Hilo ndilo tu lote linalompasa kufanya, unaona, ni kuwafanya watu kuamini hilo namna hiyo, na ni hilo tu. Kwani huwezi kuondoa neno moja Kwalo, au kuongeza neno moja Kwalo, lakini hilo ndilo afanyalo.

Watu, wakimuabudu Shetani bila kujuua, wakifikiri wanamwabudu Mungu. Kama tunavyoonywa na unabii katika II Wathesalonike kwamba... Hebu na tusome tu hilo: II Wathesalonike, sura 2. Hebu tu tuifungue kwa muda mdogo, kama ninaweza sasa hivi ningependa kulisoma hilo tu... Naamini II Wathesalonike Nina Andiko hapa na linasema...

“Basi ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu, na kukusanyika kwetu mbele zake,”

Na angalia kuja kwa Bwana na kukusanyika Kwake, kwa kuwa Mungu atawakusanya watu Wake Kwake katika siku za mwisho—kukusanyika kwa watu mbele za Bwana. Si mbele ya kanisa, mbele za Bwana. Kukusanyika pamoja mbele Zake.

“Kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe? kwa roho, wala neno, wala kwa

waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo.

Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu, na yule mtu wa kuasi...” (mtu wa kuasi, angalia alivyo sasa) “...mtu wa kuasi afunuliwe, mwana wa uharibifu;” (Huyo alikuwa Yuda, unaona.)

“Yule mpingamizi ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, ama kuabudiwa; hata Yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu.”

Huo udanganyifu wa kanisa la leo hii. Unaona, mwana wa uharibifu—ibilisi. Mwana wa uharibifu—ibilisi. Halafu watu wanamwabudu Shetani siku hii, wakidhani wanamuabudu Mungu. Lakini wanamwabudu kupitia kanuni ya imani, madhehebu yaliyoundwa na mwanadamu na kanuni za imani zilizowafikisha watu kwenye udanganyifu ulio mkuu zaidi ambao ulimwengu hujawahi kuujuua. Haidhuru kiasi gani Neno la Mungu liliyooahidiwa kwa siku hii, linahubiriwa na kudhihirishwa, bado hawataliamini. Hawataliamini.

Basi kwa nini? Tunashangaa kwa nini. Kwa nini hai... kwa nini hawaliyamin? Wakati Mungu alisema angetenda kitu fulani, naye anakitenda, na bado wanakipa kisogo, na kukiachacha. Kama ambavyo Hawa alijua kwamba kile alichosema Mungu, Mungu angetenda, lakini alikipa kisogo kusikiliza kile Shetani alichosema. Kumbuka tu, katika nyakati zingine, siku zote kimekuwa kitu kile kile. Katika kila wakati imekuwa daima kwamba Shetani hujaribu kupotosha hilo Neno kwao; akiwafanya waone wakati mwingine.

Angalia, wakati Yesu alipokuja—unaona, Shetani alikuwemo katika kundi lile la waalimu wa Kiyaudi na marabi na makuhani, akijaribu kuwaambia washike Torati ya Musa, ambapo Neno lenyewe lisema—kwamba katika siku hiyo, Mwana wa Adamu angefunuliwa. Unaona? Kwamba angejifunua Mwenyewe. Kwa hiyo walikuwa wakijaribu... kadiri ambavyo waliwaweka wa kidini, na katika Torati ya Musa... unaona aililotenda? Alikuwa akijaribu kuwaambia, “Sehemu hiyo ya Neno ni sawa kabisa, lakini mtu huyu siye mtu yule.” Unaona jinsi alivyo mdanganyifu? Hiyo ndiyo hiyo siku yenyewe hasa ya udanganyifu.

Ndivyo ilivyokuwa, na sasa ndivyo ilivyo—Shetani akiimarisha ufalme wake duniani. Hiyo ndiyo sababu yake hasa ya kufanya hilo; kwani anataka kuimarisha ufalme wake mwenyewe, kama mfanyi biashara ambaye si Mkristo. Atafanya kila njama anazoweza kukufanya uone kitu kwa njia mbaya. Kama analo kusudi fulani na faida ya binafsi katika

kukufanya wewe utende hilo, kukufanya wewe ulione jinsi hiyo, atakuonyesha kila kitu anachoweza na kukuzuia uone ukweli wa mambo, kwa sababu anajipenda mwenyewe tu. Haidhuru kiasi gani anasema uongo na kudanganya, na lo lote zaidi, ana faida ya kibinagsi. Na hiyo ndiyo sababu Shetani anafanya hili. Na ametenda kazi kupitia huduma hii kufanya hilo, kama Mungu alivyoahidi angetenda.

Sasa, alianza kwa udanganyifu wa kidini huko Edeni naye ameendelea tangu hapo. Si kwa kuanzisha kundi la Wakomunisti—Wakomunisti hawahusiani na hili. Unapaswa kuwa mwangalifu kwa kanisa, unaona. Sio Wakomunisti ambao watawapoteza walio Wateule; ni kanisa ambalo litawapoteza walio Wateule, unaona. Sio Wakomunisti. Tunajua wao wanamkana Mungu—wao ni wapinga Kristo. Hakika ni wapinga Kristo—katika msimamo wao, lakini wao sio yule mpinga Kristo. Mpinga Kristo ni wa kidini: wa kidini sana naye anaweza kunukuu Maandiko, na kuyafanya yaonekane wazi sana, kama Shetani alivyofanya nyuma kule mwanzo. Alinukuu kila kitu hata... Mungu amesema, “Msile kila mti wa bustani,” unaona, akawadanganya kabisa. Akasema, “Ndio, tweweza kula miti yote ya bustani, lakini kuna mti katikati ya bustani ambao Mungu amesema tusile, wala kuugusa, kwa sababu siku tutakopuka, siku hiyo tutakufa.”

Akasema, “Loo, hakika hamtakufa, lakini hebu niwape sababu ya Mungu kusema hili. Ni kwa sababu...” Unaona, sasa alilonukuu lilikuwa ukweli, unaona. Alisema, “Litawafungua macho yenu, na litawafanya mijue mema na mabaya. Hapo basi mtakuwa kama Mungu, kama mnaweza kulifanya.” Hilo ndilo tu analotaka kufanya, na hilo ndilo tu jambo lile lile analojaribu kufanya leo hii. Siku zote imekuwa udanganyifu wa kidini tangu mwanzo kabisa huko Edeni, na imekuwa hivyo tangu hapo.

Wakati wa Adamu ilikuwa ni udanganyifu. Wakati wa Nuhu, ilikuwa ni udanganyifu. Wakati wa Yesu ilikuwa jambo lile lile. Na sasa ni jambo lile lile! Namna ile ile—udanganyifu wa kidini.

Sasa, tutaona dunia, wakati Mungu alipokuwa anaimiliki—sasa, wakati Mungu alipokuwa anaimiliki, kisha wakati Shetani alipoichukua kwa kulikataa Neno la Mungu. Mungu wakati mmoja aliiiliki dunia. Aliiweka katika njia yake ya mzunguko. Aliiweka kuifanya itende kazi. Alifanya kila kitu—aliimiliki. Sasa, tutalinganisha hilo na...baada ya Shetani kuinyakua akaitawale.

Sasa, ilimchukua Mungu miaka 6,000. Haikumchukua muda huo wote, lakini alichukua muda huo wote. Miaka elfu sita, kwa sababu tunafundishwa kwamba siku moja Mbinguni ni miaka elfu moja duniani. Na ilikuwa miaka 6,000, ama siku sita ambazo Mungu aliumba dunia.

Sasa, ilimchukua Mungu miaka 6,000 kuifanyiza; akaipanda mbegu njema na kutoa kila kitu kwa jinsi yake. Kila kitu kinapaswa kazaa jinsi yake. Mbegu Zake zote zilikuwa njema, na kwa hiyo lazima zizae aina yake. Mungu alichukua miaka 6,000.

Hatimaye, alipoitengeneza yote, na mwishowe tukafikia makao Yake makuu ya ulimwengu katika mahali pazuri, upande wa mashariki mwa Edeni, palipoitwa Bustani ya Edeni. Mungu alifanya makao makuu ya ulimwengu katika Bustani ya Edeni, katika Misri, hapo upande wa mashariki mwa hiyo bustani palikuwepo na makao makuu. Na juu ya hali yote, Yeye akamfanya mwanawewe na mke wa mwanawewe kutawala yote. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya.

Aliwaweka watawale kikamilifu. Wangenena na pepo, nazo zingeacha kuvuma. Wangenena na mti, nao ungesogea toka hapa hadi pale. Simba na mbwa-mwitu walikula pamoja, na kondoo alilala chini pamoja nao. Hapakuwepo na uovu. Ilikuwa amani kamilifu, mapatano makamilifu; kila kitu katika ukamilifu, wakati Mungu alipoimiliki. Nayo... angalia. Alikuwa na ulimwengu Wake—alienendelea kila kitu. Alikuwa na kila kitu kikija. Kila kitu kikila mimea. Hakuna cha kufa—hakuna cha kuharibika—hakuna cha kuharibiwa hakuna... ilikuwa ukamilifu tu. Na juu yake, aliwaweka watoto Wake wapendwa—mwanawewe na binti Yake; mume na mke kuitawala.

Mungu alikuwa ameridhika sana, kisha akastarehe siku ya saba, akaziacha kazi Zake zote, akaitakasa hii siku ya saba, Sabato, kwa ajili Yake. Kwa sababu Mungu aliiangalia kila sehemu; baada ya kutumia miaka 6,000 akiifinyanga na kuitengeneza: akiifanya iwepo na akaweka milima na kufanya volkano; kuiinua milima na mambo yaliyotendeka, katika milipuko; akaikausha na akaitengeneza namna alivyotaka! napo palikuwa mahali pazuri! Hapakuwa na uzuri kama huo.

Paradiso kuu sana ya Mungu, na wale wanyama wakubwa wa kale na kadhalika, wakitambaa juu yake, na wale wanyama wakubwa—hawana dhara. Walikuwa wapole kama kitoto cha paka. Hawakuwa na cho chote hata. Hakuna maradhi, hakuna huzuni; hamna hata kijidudu kimoja cha maradhi juu ya dunia. Loo, mahali pazuri vipi—ndege wakubwa wangeruka toka mti hata mti, na Adamu aliweza kuwaita kwa majina yao, nao wangerukia mabegani mwake na kumwimbia. Loo, mahali pa ajabu vipi alipokuwa napo Mungu.

Na kisha akafanya moja ya sifa Zake kutoka kwenye mwili Wake Mwenyewe, Mungu ana sifa katika mwili Wake, kama wewe ulivyo sifa za baba yako. Na angalia, wewe ulikuwa katika babu wa babu wa baba yako. Lakini katika hilo, tuseme, tutaichukulia kama kwamba ni wewe na baba yako.

Sasa, wewe hukujuua kitu cho chote ulipokuwa ndani ya baba yako. Chembe ya uhai hutoka kwa mume. Mume ana chembe ya

damu; mwanamke analo yai. Sasa, kwa hiyo chembe ya damu inao uhai ndani yake. Na basi, ulipokuwa ndani ya baba yako, kwa kweli hukuwa na habari, lakini hata hivyo, sayansi na Neno la Mungu vinathibitisha kwamba ulikuwa katika baba yako, lakini hukuwa na habari.

Lakini basi baba alitamani kukujuua. Na kwa muungano wa kuunganika na mama, basi ukafahamika kwa baba. Sasa, wewe u sifa za baba yako. Unafanana naye, na unazo sehemu za mwili wako ambazo zinafanana na za baba yako. Sasa hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa hapo mwanzo. Kila mwana wa Mungu na kila binti wa Mungu alikuwa ndani ya Mungu hapo mwanzoni. Hukumbuki hilo sasa lakini ulikuwemo humo. Yeye alijua hilo, naye alipenda wewe uwepo, ili aweze kuwasiliana nawe, azungumze nawe na akupende na kukupa mkono.

Hutaki mwanaao mwenyewe...Je! si ni siku kuu hapo mwanaao awezapo kuja nyumbani na kuketi mezani; arudipo kutoka vitani, au kitu kingine, amepata makovu? Jinsi ambavyo utamtengenezea mlo wa jioni; utamchinja ndama aliyenona au cho chote kile, na kumwandalia? Ni mwili wako mwenyewe na damu yako, naye alikuwa ndani yako. Wakati huo hukumjua, lakini ulijua alikuwepo.

Na kwa hiyo Mungu alijua kwamba tungakuwa hapa, lakini basi alituweka katika mwili ili tuweze kufikiwa. Ili aweze kuwasiliana, akawa mmoja wetu, alipofanyika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Mwenyewe; udhihirisho wote wa Mungu.

Kwa hiyo, hilo ndilo lililokuwa kusudi la Mungu kuonyesha sifa Zake katika ushirika. Nilipokuwa ndani ya baba yangu, sikuwa na habari. Lakini nilipokuwa mwanawewe na nikazaliwa naye, nilikuwa sifa, sehemu ya baba yangu, nawe u sehemu ya baba yako. Nasi kama watoto wa Mungu, tu sehemu ya sifa za Mungu zilizokuwa ndani Yake, tumefanyika mwili kama Yeye alivyofanyika mwili, ili tushirikiane mmoja na mwingine, kama familia ya Mungu duniani. Na hilo ndilo kusudi la Mungu hapo mwanzo. Ndio, bwana. Hilo ndilo Mungu alilotaka hapo mwanzo. Alimiliki kila kitu, naye alimweka mwanadamu katika Bustani ya Edeni katika uhuru wa kutenda aonavyo vyema. Kisha akasema, "Mwanangu, ni pako." Mahali pazuri namna gani.

Mungu aliridhika sana mpaka akaenda akastarehe kutokana na kazi Zake zote. Kila mti haukutoa kamwe miiba na michongoma. Hakuna matunda yaliyoota katika mti wenye miiba—kila kitu kilikuwa kikamilifu; mbegu zote zilikuwa kamilifu. Kila kitu kilikuwa katika hali kamilifu.

Ndipo, hapo alipokwenda kustarehe kidogo, adui Yake akaingia kimya kimya kwa udanganyifu naye akaitawala kwa kufasiri vibaya mpango Wake kwa watoto Wake. Hapo alipoweka imani Yake katika mtoto Wake mwenyewe, kama

uwekavyo tumaini katika binti yako wakati anapotembea usiku na mwanamume, unapomwamini mwanaao wakati inapombidi kutembea na mvulana anayekunywa pombe au mvulana anayevuta sigara, unaona? Yeye aliweka tumaini katika mwanawewe kwamba asingefanya kitu cho chote kibaya, naye angetunza kila Neno ambalo alisema, lakini adui akaingia. Kama yule mhuni mjanja ambaye angemchukua binti yako na kuwa na adabu mbaya, au mwanamke fulani angetoka na mwanaao na kutenda kitu kile kile, unaona. Aliingia kwa ujanja, adui wa Mungu aliingia, naye akamtafsiria Neno vibaya Hawa.

Sasa, Yeye, kwa kuanguka huku, ameitwaa na kuimiliki Bustani ya Edeni, ye ye mwenyewe. Aliitwaa. Na sasa, amekuwa na miaka 6,000 ya utawala wa udanganyifu; akidanganya watu (watoto wa Mungu) kama aliviyotenda wakati huo, kwa sababu walikuwa wamebekwa kwenye uhuru wa kutenda walilolitaka, na kuamini kwamba wangetenda lililo sahihi, au kutumaini wangetenda lililo sahihi, basi wakaja na tendo lisilo sawa, na wakauza haki yao ya mzaliwa wa kwanza (kama alivyoofanya Esau) kwa ulimwengu; na Shetani alishinda, na akaichukua. Naye amekuwa na miaka 6,000 kujenga Edeni yake, kama Mungu alivyokuwa na miaka 6,000 kumaliza Edeni Yake, na kwa udanganyifu; (udanganyifu wa Neno au wa watu) sasa, aliweka Edeni yake mwenyewe humu duniani katika dhambi.

Edeni ya Mungu iliwekwa katika haki; Edeni ya Shetani inawekwa katika dhambi, kwa sababu Shetani ni dhambi. Mungu ni haki. Ufalme wa Mungu uliwekwa katika haki, na amani, na uzima; na utawala wa Shetani uko katika dhambi, na dhambi ya kidini!

Angalia jinsi alivyozipoteza katika udanganyifu kama alivyo sema angefanya. Aliahidi kufanya hili. Je! kuna mtu anayejua hilo? Hebu tufungue Isaya, kama mkitaka baadhi ya Maandiko haya, kama mki... Yanibidi ninukuu mengi zaidi, nabuni. Hebu tufungue Isaya sura ya 14 kwa muda mchache, tuone tu ambalo Shetani alisema hapa, muda kidogo. Katika Isaya, 14, tutaisoma. Na tazama jamaa huyu alilofanya. Isaya 14; anzia na aya ya 12.

“Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, ewe uliyeliangusha taifa.

Nawe ulisema moyoni mwako, nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kitu changu juu kuliko nyota (yaani wana) nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, juu ya upande wa mwisho wa kaskazini:

Nitapaa kupita vimo vyta mawingu; na nitafanana na Yeye aliye Juu.”

Sasa, linganisha hilo hapa na yale Maandiko mengine katika Wathesalonike, muda uliopita; jinsi alivyosema anaketi katika hekalu la Mungu, akijiinua mwenyewe juu ya kila kiitwacho Mungu. Ili kwamba yeche kama Mungu, anaabudiwa kama Mungu duniani.

Hapo yupo mungu wa dunia hii ambaye nimewahubirieni mnamo Jumapili iliyopita. Yupo hapa leo katika udanganyifu. Saa ile danganyifu! Wakati huu mkuu ambamo tunaishi! Ni wakati mzuri zaidi ya nyakati zote, kwa sababu tunaelekeea ule Utawala wa Miaka Elfu tena! Tunaelekeea Edeni tena. Lakini papa hapa kwenye wakati huu, (kila udanganyifu na kila ujanja ambao aliwahi kuutumia na ameweza kudanganya) ameukusanya wote pamoja na kujiimarisha, na kushuka kama Mungu, na kujiweka mwenyewe mahali pa Mungu, wa kidini, naye anaweza kunukuu Maandiko, naye anaweza kukuambia Maandiko—kama vile Shetani alivyofanya kwa Hawa katika Bustani ya Edeni. Lakini kuacha sehemu moja ya hilo ndilo lote limpasalo kutenda, kufanya pengo hilo, ambapo sumu ya fundisho la Shetani inaweza kuingilia, kama “chujio la mtu mwenye busara” ambalo tulikuwa tukizungumzia usiku ule mwingine.

Sasa, alisema atajiinua mwenyewe juu ya aliye Juu. Atapanda juu ya vimo vya mawingu na nyota, naye angeketi hapo kama Mungu, na kuwa juu ya aliye Juu. Naye amefanikiwa katika kutekeleza vitisho vyake. Bila shaka amekuwa na mafanikio ya ajabu katika kutekeleza vitisho vyake, kwa watu wakimwachilia aeleze vibaya kila kitu katika kila wakati, thamani ya Neno la ahadi la Mungu kwa wakati ule! Hivyo ndivyo alivyotenda hasa. Katika kila wakati alilieleza vibaya.

Katika siku za Nuhu, alieleza kwamba haingewezekana kunyesha mvua toka Mbinguni, kwani hakuna mvua juu huko. Injili kubwa ya kisayansi ambayo aliihubiri katika Bustani ya Edeni, aliweza kupeleka vyombo kwenye mwezi, na kudhibitisha hakuna unyevu huko! Lakini Mungu alisema mvua itakuja, lakini Shetani alifanikiwa katika kutia sumu bongo za watu kwa utafiti wa kisayansi kwamba isingewezekana kutendeka, lakini litendeka! Mungu alisema ingetendeka, nayo ikatendeka. Alitenda hivyo.

Sasa, katika siku za Yesu, alitenda jambo lile lile. Alitia sumu bongo zao tena kwa uongo, unaona—kutafsiri Neno vibaya. “Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, sasa hebu nione ukifanya kitu kuhusu jambo hilo.” Yesu hakujipumbaza kwake. Hakufanya hivyo kamwe. Mungu hajipumbazi. Si lazima ajibu kitu cho chote ambacho Shetani anauliza. Yeye tu... Yesu alisema “Imeandikwa wewe hutaishi...Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.” Unaona, Yeye haikumlazimu kujipumbaza kwake. Haikumlazimu kutengeneza mkate. Angeweza kufanya hivyo,

lakini angekuwa anamsikiliza ibilisi, na kwa hivyo haikumpasa kumsikiliza ibilisi.

Pia, ni dhambi ya kidini, kama hapo mwanzo—danganyifu sana. Liangalie sasa. Si tu dhambi ya kale ya kila siku—kuzini na kulewa, na kutumia Jina la Mungu bure. Si hiyo. La.

Mnakumbuka miaka mingi iliyopita, wengi wenu hapa, washiriki wa siku nyingi, mnakumbuka yale mahubiri niliyohubiri juu ya *Kuadhirika Hukumuni?* Kahaba, ye ye hataadhirika hapo. Anajua anakwenda wapi. Mlevi hataadhirika kule—mfanya magendo ya pombe, mcheza kamari, mwongo, mwizi—ye ye hataadhirika. Ila mtu yule anayefikiria ye ye yuko sahihi—huko ndiko kuadhirika. Huyo ndiye yule mtu, aliyekuja akasema, “Bwana, sikuhubiri Injili; sikutoa pepo katika Jina Lako.”

Yesu alisema, “Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwaja ninyi kamwe.”

Hapo ndipo penye kuadhirika, unaona—huo udanganyifu. Hilo ndilo ambalo wakati wote—hapo ndipo ambapo sieleweki sana. Si kwamba nataka kuwa tofauti. Sitaki kuwa tofauti, lakini yanipasa niwe kweli.

Nina Ujumbe, na huo lazima uende kwa watu. Hukufanya usieleweke sana mionganoni mwa watu. Wanafikiri ninapinga watu wote. Kama wangejua tu, nampenda kila mtu. Ninajaribu niwezavyo kuwalettea iliyo Kweli, kama inavyowekwa moyoni mwangu, na jinsi inavyowekwa katika Biblia, hapa. Na Mungu anathibitisha hilo kuwa Ukweli, kwa hivyo hakuna kitu kingine cha kufanya kulihusu. Ama wanaliangalia au hawaliangalii.

Unaona, hawataki kuliona, kwa sababu wamekwisha uza tayari. Wameuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza kwa taratibu fulani, dhehebu fulani, kujaribu kwa haki yao ya mzaliwa wa kwanza kufika Mbinguni juu ya msingi wa taratibu ya dini, ambayo Shetani ndiye kichwa cha kila sehemu yake.

Mungu hajawahi kuwa na dini ya kidhehebu, kwamwe hajawa nayo. Nao wanajuza kwa hiyo. Ambapo wao... kundi la watu wanafasiri Neno, na kusema linamaanisha hivi, na linamaanisha vile. Mungu hahitaji mfasiri. Hujifasiria Mwenyewe. Hahitaji mtu mwingine ye yote kumwambia namna ya kulifanya. Yeye ni mwenye uweza wote. Alisema namna angelitenda, na hivyo ndivyo jinsi inavyombidi kushika Neno Lake. Hapo aliposema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” Yeye alimaanisha hilo tu.

Lo lote alilosema lingetokea, alisema litatokea katika siku hizi za mwisho kwamba angetenda mambo fulani, na ameyatenda. Haimlazimu kumuuliza ye yote kama kuna muda au la, anajua ni muda gani, na mpango ni nini. Sasa, Shetani, huyu mdanganyifu, kama ilivyonenwa katika Mathayo 24:24 na udanganyifu mwingi mno.

Sasa, tunaona kwamba kwa mpango wake wa injili ya ujuzi: elimu bora, elimu ya maadili ya hali ya juu, ustaarabu, na kadhalika, imewaloga watu ambao wanataka kumtumikia Mungu katika kuamini uongo wake. Hawa hakutaka kufanya hilo, lakini alimwonyesha jinsi ilivyokuwa na hekima zaidi.

Yeye hakujuua. Alitaka kujuua. Hakufahamu, lakini alitaka kufahamu. Na Mungu akamwambia asijaribu kuelewa. Nawezaje kuelewa lo lote la mambo haya? Siwezi kuyaelewa. Ninayaamini. Hainilazimu niyaelewe. Mungu ni imani, na sio kuelewa. Tunaamini tu analosema.

Sasa, linganisha Edeni ya Mungu na ya Shetani sasa, baada ya miaka 6,000 ya upotovu wa tafsiri ya kweli ya Neno la Mungu lililoahidiwa kwa wakati huu. Hebu tulilinganishe sasa, na angalia ni wapi tunalipata. Kama alivyofanya kwa kanisa wakati wa Kristo, katika Yesu—akijaribu kuwazuia wana waaminifu wa Mungu kuujua Ukweli. Hiyo ni Mungu... Mungu aliaweweka watoto Wake hapa, sifa Zake, kushirikiana naye kwa kusikia Neno Lake.

Vipi kama baba yako angekuambia...nawe u mwana mwaminifu kwa baba yako. Naye alikuambia, "Mwanangu, usiende kwenye maji yale kule, kuogelea, kwa sababu kuna mamba katika maji yale." Na mtu arudi na kusema, "Hakika, maji mazuri kama hayo, hayana mamba."

Sasa, utamsikiza nani? Kama u mwana kweli kweli, atamsikiliza baba yako. Na mwana halisi au binti wa Mungu huchukua Neno la Mungu kwanza! Sijali ambalo mtu mwingine ye yote anasema kuhusu hilo, wanaamini Neno la Mungu kwanza. Kuna sumu katika kikombe, nao huamini hilo. Kuwa na imani katika Neno Lake lote, Mbegu Yake, kulileta Edeni ya utakatifu, upendo, na Uzima wa Milele!

Hilo ndilo ambalo Edeni ya Mungu inatoa—utakatifu, nayo ililetla Edeni ya utakatifu, upendo, ufahamu, ukamilifu, na Uzima wa Milele. Hilo ndilo analopanda Mungu; Neno Lake, Uzao Wake, hivyo ndivyo Kanisa Lake litakuwa mwishoni. Litakuwa kitu kile kile.

Angalia, pana wazo hapa. Usilisahau. Nitalifikia wakati mwingine, au ujumbe mwingine, lakini unajua, Mungu alisema, "Kila mbegu itoe kwa jinsi yake." Hiyo ni amri ya Mungu? Sasa, itamfaa nini mhubiri ye yote au mtu mwingine ye yote kujaribu kulifanya Neno lile liseme kitu kingine? Unaona? Kila Neno la Mungu ni Mbegu. Yesu alisema hivyo—mbegu aliyoipanda mpanzi. Kwa hiyo, kama Marko 16 ni Neno la Mungu, litazaa kwa jinsi yake. Kama Malaki 4 ni Neno la Mungu, litazaa kwa jinsi yake. Na kila ahadi nyininge lazima izae kwa jinsi yake.

Unaona? Unamuona Shetani hapa katika kujibadilisha? Anajaribu kusema, "Sio hivyo." Mnaelewa hilo? Unaona, Shetani asema, "Loo, hilo si la siku hizi. Hilo ni la wakati

mwingine. Hilo hata halimaanishi hilo.” Kila mbegu lazima izae kwa jinsi yake! Hivyo ndivyo ambavyo Mungu aliimarisha Edeni yake. Sivyo?

Na ndilo hili hapa. Hivyo ndivyo ambavyo Mungu huliimarisha Kanisa Lake. Kila Neno kwa jinsi yake. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno linalotoka kinywani mwa Mungu,” unaona. Shetani, atachukua kitu kingine, lakini Mungu alisema, “Kila mbegu kwa jinsi yake.” Kama ahadi ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, kanisa husema, “Junge na kanisa, kariri kanuni za imani, ijue katekisimo.” Hakuna mambo kama hayo katika Biblia nzima! Lakini, Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu, watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Kama wakishika nyoka, au wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ni mtu gani atakana hilo? Unaona?

Kila mbegu itazaa kwa jinsi yake. Kama wewe ni uzao wa Mungu, sifa, mwana wa Mungu, basi Neno la Mungu limepandwa ndani yako, unaona. Na basi unapolisikia Neno la Mungu—“Kondoo Wangu huisikia sauti yangu; mgeni hawatamfuata.” Unalipata? Basi kila mbegu hutoka kwa jinsi yake.

Sasa, tunaona kwamba kila mbegu ikizaa kwa jinsi yake, hapakuwa na kifo katika Edeni ile. Hapakuwa na kifo katika Edeni mpya, unaona. Hapakuwa na cho chote kingine isipokuwa utakatifu, usafi, na Uzima wa Milele.

Sasa, kwa kutokuamini katika Neno lote la Mungu kumeleta mbegu ya *uchafu* katika Edeni ya Shetani. Sasa tunaingia ndani ambapo Shetani amechukua kiti cha enzi kama mpinga Kristo katika Edeni ya dunia hii, Edeni ya dhambi—dini iliyopotoshwa. Alianza, si katika: “Mimi ni Shetani. Mimi ni yule malaika mkuu.” La, si katika hilo, lakini kwa kulipotosha Neno la Mungu! Na hivyo ndivyo alivyoleta utawala wake katika kila wakati. Na sasa katika wakati huu mkuu wa udanganyifu, tayari kuchukua kiti chake cha enzi kwa watu wake! Amejjengea Edeni ya kiakili, ya elimu, ya kisayansi. Sawa. Wahubiri wa kisayansi, kanisa la kisayansi, theologia ya kisayansi—kila kitu ni cha kisayansi. Kila kitu kiko kwenye msingi wa ujuzi. Kanisa lote limejengwa juu ya ujuzi. Halikujengwa juu ya imani.

Wakati mmoja nilikwenda kufanya mkutano kwenye kanisa la mtu fulani. Lilikuwa jumba kubwa la mikutano huko magharibi. Mtu mzuri—naye alikana vitu hivi ambavyo tunazungumzia. Hata hivyo, nilimpenda. Mtu mzuri—mzee. Kusanyiko lake lilipotoka...liliketi watu 6,000. Kusanyiko lake lilipotoka nje katika ibada ya alasiri (kama 1,500) wote walikuwa wasomi waliovalia nadhifu nami niliketi pale na kuwaangalia. Alihubiri mahubiri mazuri sana—mtu huyo

alihubiri. Na halafu aliuliza kama ye yote alitaka kumkubali Kristo; wainue tu mikono yao. Na hakuna aliyeinua mkono wake. Hata hatimaye mwanamke mmoja akainua mkono wake.

Akasema, “Vema, sasa u Mkristo,” na akamweka kwa ubatizo. Na kisha akatoka; akamweka wakfu mtoto mchanga, (akambusu mtoto mchanga) na kumuombea, na akatawanyisha kusanyiko.

Kusanyiko lake lilipotoka—wote ni watu wazuri, waliosoma, walioelimika, kisha nilikuwa nimesimama kando kumpa mtu huyo mkono, na kumtakia mafanikio kwa Mungu, alipokuwa akitoka. Na nilipoingia, hapa kundi langu likaingia. Hawangewaruhusu kuungia wakati kundi lake lilipokuwa pale. Hapa laja langu katika magari ya kusukumia wagonjwa, machela, makoti ya wakichaa, wenda wazimu na kadhalika. Unaona tofauti? Ndio hilo. Hicho ndicho kitu ninachozungumzia, unaona. Unaona? Ni kitu tofauti.

Ambapo kwa ujuzi wa kisayansi, unaweza kufanya injili ya kueleweka—“Yeye amwaminiye Yesu Kristo hatahukumiwa,” waona, “bali ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Unaona, anashindwa kuweka hilo ndani hapo, waona. Yeye alimwamini Yesu Kristo. Ameokolewa, kama ishara hizi hufuatana na mwamini. “Na yeye alisikiaye Neno Langu,” si kujifanya kitu fulani—si kulisikia na masikio pekee, lakini kulielewa. Ye yote unaweza kulisikia.

Kahaba anaweza kulisikia na abakie kahaba, mnaona, mlevi anaweza kulisikia. Mwongo anaweza kulisikia, na bado abakie mwongo, lakini, “Yeye afahamuye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka ana Uzima wa Milele.” Ndivyo hivyo, unaona. Na hakuna mtu awezaye kutenda hilo isipokuwa Mungu amemchagua tangu zamani.

Yesu alisema “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na baba Yangu, na wote ambao Baba amenipa watakuja Kwangu.” Amina! Yote yako katika mamlaka ya Mungu, na kujua kwa Mungu tangu awali. Yeye huishi peke Yake, na hakuna mtu amuambiaye la kufanya.

Sasa, kwa kutoamini na kuchukua Neno lote la Mungu, kumeleta mbegu ya kutoamini, uchafu, ya dhambi, chuki, na kifo cha milele kiko katika wakati huu wa dhambi, wa kanisa la kiakili. Je! mmeefahamu? Siku hii, ambapo ulimwengu mzima ni wa kidini. Mlijua hilo? Ulimwengu mzima ni wa kidini. Na katika wakati huu wa kidini—makanisa makubwa kwenye kila kona. Kila kitu...jambo zima huishia kwenye kuabudiwa kwa Shetani. Hapa lipo papa hapa kwenye Biblia. Hilo ni kweli.

Na katika hizi seminari za kiakili, na za kitheologia ambazo zimezaa mtu wa bongo nydingi ambaye amefundishwa jinsi ya kuzungumza, ya kufanya, namna ya kushikwa na mshtuko wao, na kila kitu kama saikolojia—miaka mitatu na minne kujua jinsi

ya kushughulika na akili ya mwanadamu. Unaona, ni...Roho wa Mungu si kitu ambacho unaelimishiwa. Ni kitu ambacho kimewekwa ndani yako tangu awali kwa mkono wa Mungu Mwenyezi. Hauwezi kuelimishiwa ama kufunzwa ujuzi wako; umepewa huo tangu awali kwa mkono wa Mungu na kujua Kwake tangu awali. Hilo ni kweli.

Sasa, aileta Edeni hii kubwa ambayo sasa wanaishi ndani yake—Edeni ya kanisa la ulimwengu. Wote wanaunganika pamoja, sasa, kwenye Halmashauri kuu ya Ekumeni, nao watakuwa na kanisa la ulimwengu—wote wakija chini ya kiongozi mmoja ambapo Shetani atatawazwa, kweli kabisa.

Na mwito wa mwisho unatoka kumshika Bibi-arusi kabla hajaingia katika hiyo. Kwani mara aingiapo katika hiyo, amekwisha chukua Alama ya Mnyama, na amekwisha. Hatatoka kamwe katika hiyo. Hiyo ndiyo sababu ninasema, “Tokeni kwake, watu Wangu, kabla halijaenda kwake, unaona. Tokeni kati yao, mkatengwe nao.”

Sasa, chuki na kifo, na kutengwa milele na Mungu katika Edeni hii—tamaa mbaya, uchafu, upotovu. Vipi?—kwa kupanda mbegu mbaya.

Inanikumbusha ono nililoona kabla sijakutana na Wapentekoste, ya mtu yule aliyezunguka ulimwengu amevaa mavazi meupe. Mmenisikia nikilisimulia mara nydingi. Mmoja akaja nyuma yake akipanda mbegu za kutopatana, lakini alishinda kwa urahisi, katika Hawa (katika Bustani ya Edeni) kwa tamaa mbaya ya Hawa ya dhambi—tamaa mbaya ya Hawa ya kutenda dhambi.

Basi kama Hawa alitamani maarifa, ilikuwa dhambi. Nasi tunapotamani maarifa (tunataka Ph.D, LL.D.) ni dhambi kufanya hivyo. Huo ni msemo mzito, lakini hiyo ni Ukweli. Haidhuru ni mzito kiasi gani, bado ni Ukweli, mnaona. Kutamani maarifa, ufahamu... Jambo lenyewe ni kwamba, ni leo hatujaribu kuliimarisha Neno la Mungu katika mioyo ya watu. Tunajaribu kuijimarisha sisi wenyewe! Makanisa yanajaribu kuweka fundisho la kanisa katika moyo wa mtu. Tumeamriwa kuliimarisha Neno la Mungu. Paulo alisema, “Sikuwajia kwa maneno ya hekima yenyeye kushawishi akili za watu ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, lakini naja kwenu kwa nguvu; katika madhihirisho ya Roho Mtakatifu ili imani yenu ikae katika Mungu.”

Haya basi. Wanadamu lazima wajiiamarishe wenyewe. Tunaliona mionganoni... Hebu Mungu na atende kitu kwa mtu na amtume, utaona kila mtu akijaribu kumuigiza. Unaona, wanajaribu kuijimarisha wenyewe. Kila mtu “Nilitenda hili, *mimi, mie*, dhehebu *langu*, *mimi* hili”—wakijiimarisha wenyewe. Tunahubiri juu ya nini, sisi wenyewe, au ufalme wa Mungu? Liimarisheeni Neno la Mungu. Ondoeni kutoamini kisha muweke

ufalme wa Mungu katika moyo wa mwanadamu. Na ufalme wa Mungu hauwezi kuimashwa katika moyo wa mwanadamu isipokuwa Mungu amemuumba mtu huyo namna hiyo. Hawezi kuwekwa katika . . . na kumbuka, sehemu iliyodanganyifu ni kwamba, mtu huyo anafikiria kwamba ni sawa. *"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu huyo."* Kila mtu mwenye akili nyingi huonekana wa kweli.

Kama nilivywambia Jumapili chache zilizopita; niliposimama karibu na mtoto wangu mchanga aliyekuwa anakufa, na Shetani akisimama hapo na akasema, "Baba yako yuko pale—alifia mikononi mwako usiku uliopita. Mkeo yupo pale amelala katika chumba cha maiti; na mwanao yupo hapa anakwenda, na unamwomba akujibu, na ameshusha kivuli juu yako. Na sasa, bado Yeye ni Mungu aliye mwema, na bado ulisema alikuwa Mponyaji. Nawe, ambaye unasimamia kile ulichosema ni sawa, umekosea."

Loo, kila sababu, kila sehemu ya akili ilibidi ikubaliane kwamba ilikuwa sahihi, na ye ye alikuwa sahihi, kiasi hicho.

Vivyo hivyo alikuwa sahihi alipomwambia Hawa, "Macho yenu yatafumbuliwa, nanyi mtajua yaliyo mema na mabaya, nanyi mtakuwa kama miungu namna hiyo," (mkijua mazuri na mabaya) kwa sababu Mungu hakuwaruhusu wajione wenye we bado, kwamba walikuwa uchi. Kwa hiyo walijua wangejua mema na mabaya. Naye alikuwa sahihi! Lakini, unaona, ilikuwa kinyume cha Neno la Mungu.

Vivyo hivyo wahudumu katika seminari wakijifunza theologia za mwanadamu. Yawenza ionekane sawa, yawenza iwe fahamu nzuri ya jambo hilo, lakini ni makosa! Haitubidi kulielewa. Tunaliyamini, kwa sababu Mungu alisema ndivyo ilivyo, na hilo latosha milele— jambo hilo lote. Hivyo ndivyo tunavyoliyamini. Loo, jinsi Hawa alivyotamani kupata Ph.D.— jinsi alivyotamani kuwa na akili kuliko alivyokuwa.

Angalia, jinsi walivyofanana mtu na mkewe . . . Sasa angalia, mtu na mkewe, wote wawili uchi katika Bustani ya Edeni, Edeni ya Mungu . . . Sasa nitamalizia, nilisema nitaendelea kwa dakika chache. Angalia. Tazama sasa, katika kufunga. Linganisha hili sasa. Kiasi gani wanavyofanana mtu yule na mkewe, wote wawili katika Edeni ya Mungu, bila kuva kipande cha nguo kilichoshonwa, na hawakujua. Kwa nini hawakujua? Kwa kuwa walikuwa wamefumbwa hisi zao za kujijua wako uchi kwa Utaji Mtakatifu wa Roho Mtakatifu. Waliweza kutazamana, na hawakujua kwamba walikuwa uchi. Walikuwa wametiwa utaji na Roho Mtakatifu wa utakatifu. Walikuwa wametiwa utaji.

Utaji wa Mungu, hata leo, unaweza kuangalia na usitamani. Wanageuza vichwa vyao. Ni Utaji Mtakatifu, unaona. Utaji Mtakatifu. Macho yao yalikuwa na Mungu. Wote wawili walikuwa . . . mmoja alikuwa mwanamume na mwingine

mwanamke, nao hawakujua walikuwa uchi, kwa sababu Utakatifu wa Mungu uliyafunika macho yao. Angalia. Mungu alificha dhamiri zao kutoka kwa dhambi kwa Utaji Mtakatifu. Laiti tungelikuwa na wakati kuangalia hilo dakika chache.

Angalia hapa, "Kwa maana yeye, mwabudu akisha kusafishwa mara moja . . ." (Waebrania) "mwabudu akisha kusafishwa mara moja asingejiona tena kuwa na dhambi." Dhambi imeondolewa mbali naye!

Nilimsikia Ndugu Neville akisema asubuhi hii, pengine mtu fulani alikuwa akimuuliza, "Kwa nini sikuhubiri juu ya Roho Mtakatifu? Kwa nini sikufanya jambo hili?" Hili hapa. Roho Mtakatifu ni matendo yaliyo ndani yako. Ni Uzima. Si msisimko wa mwili; sio namna fulani ya uhakika wa matendo ya kimwili, bali ni Mtu, Yesu Kristo, Neno la Mungu lililowekwa katika moyo wako kuhuisha kila neno la wakati huu. Sawa. Muangalie Roho Mtakatifu katika matendo, si sana katika dhihirisho lakini katika matendo—anavyotenda kulingana na Neno.

Angalia, sasa, Roho Mtakatifu wa Neno Takatifu la Mungu alimweka mwanamume na mwanamke uchi, na hawakujua. Ni zuri jinsi gani—uzima wa Neno, mbegu, lile Neno. Mungu alisema, "Kuna mti katikati ya bustani, (mwanamke). Na katikati ya bustani kuna mti huu. Hata msiuguse, kwa maana siku ile mtakapoula, siku hiyo mtakufa." Walikuwa wametiwa utaji mtakatifu wasiuone—hawakujua cho chote kuuhusu, hawakuthubutu kuugusa.

Walikuwa wametiwa "utaji mtakatifu." Walikuwa salama katika hema kubwa ya Mungu. Walikuwa hai. Hawakuwa na vifo kila mahali. Haleluya! Walikuwa na upendo mkamilifu mmoja kwa mwenziwe, Uzima mkamilifu milele, walikuwa na upendo mkamilifu, ufahamu mkamilifu wa upendo wa Mungu. Walikuwa na Neno la Mungu, na walilishika. Nao walikuwa hai na salama katika Edeni ya Mungu bila ya kifo kamwe kila mahali.

Basi, Shetani akamfanya Hawa kusikiliza injili yake ya theolojia— injili ya maarifa, kisomo cha juu, maadili ya hali ya juu, ustaarabu bora, elimu ya juu, na kadhalika. Basi, alipofanya kusimama na kumsikiliza kwa dakika moja, (hoja zake, ambazo tunaambiwa tuziangushe) alipomfanya azisikilize—"Sasa, tazama hapa. Kanisa liko hivi na vile. Limekwisha kuweko kwa muda mrefu. Sisi tu kanisa majawapo la kale sana nchini. Meya wa mji huenda . . ." Sijali ni nini, unaona. Kama ni kinyume cha Neno la Mungu, lipinge. Huyo ni adui wako. Kitu cho chote dhidi ya Neno ni adui wako. Kila kitu ambacho hupenda Neno ni ndugu yako. Yeye ni sehemu yako.

Angalia, aliondoa ule Utaji Mtakatifu ili aone jinsi kujuana kimwili kulivyo hasa; (linganisha hilo) jinsi tamaa mbaya ingefanya. Aliondoa ule utaji machoni pake. Kile kitu kitakatifu

ambacho Mungu alikuwa ameweka machoni pake, alitaka maarifa ajue ilivyokuwa. Kwa hiyo, aliondoa ule utaji apate kuona ilikuwa nini. Alimsikiliza ibilisi, basi angalia alimwingiza mahali pa namna gani.

Wametenda jambo lile lile katika kila wakati, baadaye—siku zote wakienda upande wa akili. Na sasa wamejenga ufalme wa maarifa ya Shetani (mbegu yake aliyopanda) nayo imeufanya ulimwengu kuwa Edeni ya kifo.

Sasa, angalia. Sasa tazama Ufunuo 3, Wakati wa Kanisa la Laodikia. Lifikirie bongoni mwako. Sasa, angalia. Yeye, Hawa, ni malkia wa Shetani. Unaona, Shetani (yule nyoka) alimfikia Hawa kabla Adamu hajamfikia. Unaona. Hilo ni kweli. Kwa hivyo alimdanganya—kwa hivyo Shetani, yule nyoka alikuwa mume wa Hawa kabla ya Adamu kumjua. Unaona. Alimdanganya. Biblia ilisema alimdanganya, naye akajua alikuwa uchi, saa hiyo. Unaona?

Sasa, utazame wakati wa Kanisa la Laodikia. Yeye, Hawa, ameketi kama malkia wa Shetani. Yu tajiri katika mali ya dunia, kipofu, uchi tena, na hajui hilo! Kama tu ilivyokuwa katika Edeni ya Mungu. Lakini sasa, si kwa sababu ule Utaji Mtakatifu umo juu ya uso wake, lakini utaji wa tamaa mbaya, ambapo aliondoa ule Utaji Mtakatifu wa Mungu, na akavaa utaji wa ujuzi kwa ajili ya tamaa mbaya. Na sasa ana utaji wa tamaa mbaya hata yu kipofu kwa jambo hilo kuwa ni dhambi. Yuko uchi barabarani, naye hajui hilo. Yeye ni kahaba mitaani. Wanawake waliovaa kaptura hizi usoni pa Mungu ni kahaba, nao hawajui hilo.

Angalia, chukua wanawake wetu. Sasa, kama ukitaka kuona hali ambayo kanisa limefikia, angalia namna wanawake wanavyoenenda. Mwanamke siku zote huwakilisha kanisa. Katika Edeni ya Shetani ya dhambi na kutoamini—upotovu wa kidini; ufalme uliopotoka. Badala ya kuchukua Neno la Mungu, wamechukua akili ya kisomo ya binadamu. Badala ya kuchukua Kanisa, wamechukua dhehebu, na wanaliletka kwenye kiongozi mmoja mkuu.

Sasa angalia, wamepotoshwa kutoka kutokuwa na hatia... Usikose hili sasa. Kanisa limevaa utaji huu wa tamaa mbaya. Angalia kile ambacho hilo limelitendea. Limelipotosha toka kutokuwa na hatia likapata maarifa. Unaona. Ule Utaji Mtakatifu, hakuwa na hatia; akiwa na ule utaji wa tamaa mbaya, yeye ni maarifa. Anajua ni wa kupendenza. Anajua kile unachofanya, waona. Ni tunda, mti wa kutamanika, kumpa mtu maarifa. Unaona. Amepotoshwa kutoka kutokuwa na hatia akapata maarifa, kutoka utakatifu hadi uchafu na tamaa mbaya, na toka Uzimani kuingia mautini.

Ufalme huu lazima ufe! Ufalme huu utakufa! Mungu wa Mbinguni atauharibu toka uso wa nchi!

Angalia katika upotovu huu, umetoka kwa mwanamume hadi mwanamke na kutoka mwanamke hadi mwanamume na hawajui hilo! Tunda zuri sana la Edeni ya Shetani kama utatazama barabarani leo hii, uwaangalie watu wetu wa kisasa.

Angalia, ilikuwa Hawa ambaye Shetani alimtumia kumfanya Adamu atende dhambi kwa nguvu zake za tamaa mbaya. Sasa, vivyo hivyo, akifanya kitu kile kile leo. Angalia, nywele zilizokatwa, nyuso zilizopodolewa, nguo za kutamanisha, unaona. Yeye hutenda hilo, na hajui kwamba kila moja ya mambo hayo ni kinyume cha Neno la Mungu! Kukata nywele zake, humfanya mwanamke asiyé na heshima—kahaba. Kuvala kaptura, humweka katika aibu. Kuvala mavazi ya kutamanisha, humfanya kahaba, naye hajui hilo! Si kwa sababu ya utakatifu wa Mungu; kwa sababu tamaa mbaya ya Shetani!

Alimfanya Adamu wake... Alimfanya Adamu wake amtamani. Alivua zile nguo ambazo Mungu alimvalisha, kule nyuma katika Edeni, kwa safari yake katika hili jangwa—aliziondoa. Alijivua nguo, ambapo Mungu alikuwa amemfunika kila mahali kwa ngozi; ameanza kukata nywele zake kidogo-kidogo kila wakati. Sasa, amerudi ambapo alikuwa hapo mwanzo. Sasa, amemfanya Adamu wake avae nguo zake za ndani.

Mwanamume, akivaa hizo kaptura, zinazofanana na za kike, na kutoka nje huku. Sidhani kuna uanaume wa kutosha kwake. Ndiye jike kuu sana ninalojua. Unaona, amemfanya Adamu wake aliyepotoka kutenda kama anavyotenda yeye. Unaona? Kuvala nguo zake za ndani. Aliona aliloweza kufanya huko nyuma, wakati alipovua nguo zake, bali nguo zake za ndani—hizo ni kaptura bila shaka, hizo ni nguo za ndani za mwanamke.

Na hapa Adamu wake anazivaa, sasa. Ambalo, kulingana na Neno la asili la Mungu ni chukizo kwa mwanamke kuvala nguo zimpasazo mwanamume, na mwanamume akivaa nguo zimpasazo mwanamke, kutoka Neno la asili. Fikiria hilo.

Sasa, mwanamume sasa anakata nywele kukingama uso kama mwanamke, pia. Anazichana na kuzitia vifingirisha nywele. Baadhi ya mambo ya kuchafua moyo sana niliyowahi kuona maishani mwangu ni baadhi ya watoto hao hapa leo wamekata nywele zao kukingama uso na kuzichana nyuma hivi, na nywele zilizotiwa rangi na namna fulani ya dawa ya peroksaidi na kuitia rangi, na kuziviringisha katika vifingirisha nywele wakizikingamisha usoni. Mwanamke mkubwa we! Hicho ni kitu kibaya sana kuzungumzia mimbarani, lakini hukumu huanzia kwenye nyumba ya Bwana. Hata hujui kama wewe u mwanaume au mwanamke. Tena nasikia kwamba Jeshi letu la Marekani litavaa kaptura hivi punde. Hilo ni kweli. Unaona huo upotovu ulivyo? Ni nguo za wanawake—anakata nywele kukingama uso kama mwanamke.

Hivi majuzi nilikuwa huko kwa Howard Johnson, si huyu aliyeo hapa bali ni yule aliyeo kwenye barabara ukitoka, na niliketi tu katika ushangao. Hapa yuaja mvulana mdogo, mdomo wazi. Na alikuwa na nywele nyeusi hapa, naye alizichana upande huu, na kuweka kifingirisha, na akazifingirisha juu ya macho yake; akitazamia juu ya macho yake, akienda huku na huko... Kama niliwahi kuona upotovu.

Unaona, asingalilamin. Angeweza kuthibitisha labda alikuwa mwanamume, lakini katika roho yake yeche ni mwanamke. Hajui ni wa upande gani wa nyumba. Hilo ni kweli. Jinsi alivyopotoshwa! Hilo ndilo ambalo Shetani anafanya! Hupotosha mataifa. Hupotosha kanisa! Hupotosha watu! Ni mdanganyifu—mpotoaji wa Ukweli wa asili. Mungu alimfanya mwanamume mwanamume. Alimfanya mwanamke mwanamke, na aliwavalisha tofauti, na alimaanisha wabakie namna hiyo na kuenenda namna hiyo. Mmoja ni wa kike, na mwengine ni wa kiume. Alimtenga Adamu katika Bustani ya Edeni na akafanya hili; akamtenga Hawa kutoka kwa Adamu.

Sasa, yeche hukata nywele kukingamisha uso kama za mwanamke, kukata nywele zake kama za mume, na mwanamume hujaribu kuwa na nywele kama za mwanamke. Mwanamke huvaa nguo za mwanaume za nje, naye mwanaume huvaa nguo za mwanamke za ndani. Sasa, hilo laonekana jambo la ukufuru, lakini silimaanishi namna hiyo. Ni Ukweli kabisa wa Injili. Kama hulijui hilo, basi una kasoro. Ama wewe u kipofu au hujapita barabarani. Naye mwanamke na mwanamume pia hufikiria kwamba ni sahihi. Wanapatana mahali fulani.

Wanawake husema, "Vema, ni joto sana." Wazee wa Kihindi wa Apache kule wangewaaibisha. Kadiri wanavyopata joto, ndivyo wanavyovaa nguo zaidi—kujikinga na juu. Kukufanya utoke jasho kusudi upate kubaridishwa wanapotembea. Wao husimama kule nje juani. Usingeweza kuvumilia cho chote, ungetoka uvimbe kutokana na joto kali na kuungua. Bali, unaona, ni kile wanachoita elimu ya juu. Sayansi ya kisasa imeleta hili.

Loo, jamani, huyo hapo uchi katika Laodikia, na hajui hilo. Alikuwa uchi huko Edeni. Unaona hizo falme mbili zinafanana? Mmoja ni wa dhambi na kifo. Ule mwengine ni Uzima na haki. Ndani humo alitiwa Utaji Mtakatifu. Wote wawili walikuwa uchi. Hawakujua hilo. Hawakujua cho chote kuhusu hilo, kwa sababu walikuwa wametiwa utaji wa Roho wa Mungu.

Na hapa wamevaa vazi la tamaa mbaya, na wanatazamana ku... Unaona, Adamu aliweza kumtazama Hawa, na hakujua kwamba alikuwa uchi. Lakini, sasa akiwa na vazi hili la tamaa mbaya, hatambui kwamba yu uchi, lakini analitenda hilo chini ya huu utaji wa tamaa mbaya kumfanya mwanamume amtazame. Ndilo jambo pekee linaloweza kumfanya atende

hivyo. Huamini hilo, lakini unalitenda hata hivyo. Na mwanamume anaangalia. Na aliona kwamba unavutia sana, mpaka akaja na kucaa baadhi ya nguo zako juu yake mwenyewe.

Loo, upotovu jinsi gani. Ni wakati wa namna gani. Ni muhula wa namna gani. Jinsi ulivyo mdanganyifu. Loo, mambo haya yote na hajui jambo hilo—roho iliyopotoka kabisa imo ndani ya mwanamume. Ametiwa utaji wa tamaa mbaya ya Shetani, na mwanamke, pia. Ni roho wa Shetani wa jamii kuu, unaona.

Hawajui, lakini wao ni shirika. Wanawake waliovaa kaptura ni wa taratibu za kidini. Wanaume huvalia namna hiyo... wamo katika shirika. Nitawapeni ufupi wake: C.W.W.—Chama cha Wadada Wanene. Kwa hiyo, wao ni wanachama wake. Wanakuja huko na chama cha wadada wanene na maskini suruali ndogo, kitu kinachoonekana kichafu na cha kale chenye mafundofundo.

Ewe Mwanamume, huenda usikubaliane nami juu ya hili, lakini huo ni Ukweli. Umekwisha potoshwa nawe hujui hilo. Wewe hu... hutendi tena kama mwanamume, unaona. Wamekuwa wadhaifu sana, hivi karibuni hawatakuwa na cho chote ndani yao tena—wanaume kwa wanawake, pia. Wao ni chama. Wao ni shirika. Kwa nini? "Jirani yangu Yohana anavaa kaptura, basi kwa nini mimi nisivae? Luella alitaka nizivae, kwa sababu jirani yangu Yohana alizivaa. Na, vema, kama Susie Jane anaweza kuzivaa, vivyo hivyo na Martha Jane, ama Susie Lou," ama ye yote yule, unaona. Unaona, ni chama. Ni shirika. Wewe ni mwanachama wake kiroho na huna habari.

Na kama hilo ni kweli, na twaona ni kweli, kwa hiyo wewe umepofushwa! Umepofushwa kwa madhehebu haya ambayo Shetani amekupindapinda kwayo, unaona. Ni upotovu wa Neno la asili la Mungu, Ufalme Wake, na mpango Wake kwa watoto Wake! Shetani amewapindapinda mwanaume na wanawake katika mambo haya, nao hawajui hilo—upotovu. Si mwana wa Mungu tena—nywele zilizokingama uso zikining'inia usoni mwake na kucaa kaptura na kuzurura-zurura barabarani, mwana wa Mungu? Shemasi kanisani, mchungaji mimbarani? La. Huyo si mwana wa Mungu!

Hukupitia kamwe katika chujio la mawazo la Mungu. Asingevaa hizo nguo za wanawake. Bila shaka hangalizivaa; wala yeye hangalivaa nguo za mwanamume, unaona. Si mwana wa Mungu; ni mwana wa Shetani, na binti ya Shetani. (jambo zito kulinena) Shetani amefanikiwa katika kupotosha na kuuchukua ulimwengu huu, na kuufanya ufalme wake ambamo wanadamu waliwekwa kwa uhuru wa kuchagua la kutenda wao wenyewe aina ya maisha waliiyoyatamani. Hilo huonyesha nini kilicho ndani ya moyo wako. Unaona. Sauti yako... Wajua nini? Matendo yako hunena kwa sauti kubwa sana, hata sauti yako

haisikiki. Hebu niende kwa mwanamume na kusema, "Loo, sote tu Wakristo. Tu wa kanisa," huku picha za wanawake walio uchi zikining'inia kila mahali kwenye ofisi yake? Atakachoniambia hakitaleta tofauti, ningejua bora zaidi; na wewe pia.

Kuacha mwanamke asema ye ye ni Mkristo akiwa na nywele fupi? Unajua zaidi ya hayo, unaona. Ndio bwana. Hebu na aseme ye ye ni Mkristo akiwa amejipaka rangi na poda, na kaptura, na kusema ni Mkristo? Unajua zaidi ya hayo. Neno la Mungu ukufunza mambo bora zaidi. Neno husema hawezi kufanya hivyo na awe Mkristo. Pia hata hana heshima na kila kitu. Je! Mungu atawekaje kitu kinachotahayarisha katika Ufalme Wake? La, bwana. Hata kidogo. La, bwana. Wao wenyewe—inaonyesha tamaa zao.

Huwezi kumweka hua kula pamoja na kengewa—hata kidogo. Hua hana nyongo. Hawezi kula mzoga ule wa kale. Kama akiudonoa mara moja, ungelimuua, naye anajua hivyo, lakini kengewa anawenza kula karibu cho chote anachotaka kula, unaona. Ana nyongo nyingi sana. Kwa hivyo, hapo unaona, hivyo ndivyo ilivyo na ulimwengu leo—kitu kile kile. Wako uchi, vipofu, na hawajui hilo. Shetani alifanya hivyo kwa tamaa ya mwanamke ya kupata maarifa, ya kujuana kimwili, ambayo alijichagulia mwenyewe.

Sasa, angalia, ilikuwa Hawa aliywongoza Adamu kwenye makosa, na ilikuwa mwanamke aliyevua nguo zake kabla ya Adamu wake kuvua zake. Unaona. Ni mwanamke—siku zote. Imekuwa hivyo daima. Hata sasa mambo ni kama hayo.

Kanisa ndilo linalompoteza mwanadamu. Ni kanisa, waona, ambalo humwongoza mwanamume anayetaka kuwa mwana wa Mungu; ni mwanamke, kanisa. Si Biblia, Mungu; kwani Biblia ni mwanamume. Loo, ndio, Neno lilifanyika mwili, na Yeye alikuwa mwanamume. Biblia ni mwanamume; kanisa ni mwanamke, unaona. Si kanisa . . . Biblia ambayo inampoteza mtu. Kanisa ndilo linalompoteza. Kanisa ndilo lililomfanya kwenda uchi, si Biblia. La hasa. Biblia humwambia yu uchi. Ndio bwana.

Sasa, angalia ambavyo kwa kujuana kimwili (tamaa mbaya ya kujuana kimwili) alitamani maarifa kujuua hiki kilikuwa ni nini, na jinsi tunda hili kilikuwa zuri au la, naye alilitenda.

Mungu ataurudisha hata hivyo siku fulani, kwa mwanamume. Ulitolewa na mwanamke, lakini ulikombolewa na mwanamume. Mwanamume, Yesu Kristo, ambaye ni Neno. Na basi ni kitu gani? . . . (angalia katika kumalizia) Hapa si muda mrefu uliopita, nilitoa tamshi hili. Nina kurasa kama nne au tano ndani hapo, lakini mimi . . . za Maandiko na mambo niliyotaka kuyataja, lakini sikizeni. Hebu tufunge kwa kusema hili.

Mnakumbuka hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiwafundisha juu ya zile Baragumu Saba, Sikukuu ya

Tarumbeta, na kadhalika? Na nilisema, "Kuna karamu ya siku ya nane." Kwa hiyo, siku ya saba ingekuwa ya mwisho; hiyo ingekuwa ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini kuna sikukuu ya siku ya nane, ambayo kama ilikuwa ya nane, na kuna siku saba tu, itafanya siku ya kwanza tena—kurudi nyuma moja kwa moja hata kwenye siku ya kwanza. Basi baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu kumalizika, basi patakuwepo na Edeni iliyowekwa tena. Ufalme mkuu wa Mungu utarudishwa, kwa sababu Yesu aliupigania dhidi ya Shetani katika Bustani ya Gethesemane, na akainyakua Edeni, ambayo amekwenda kuiandaa huko Mbinguni kurudi tena.

Huko Mbinguni, Yeye alisema, "Msifadhaike miyoni mwenu." Alipokuwa hapa duniani. Alisema, "Ninyi Wayahudi, mnamwamini Mungu, ('Sasa, najua nina jina baya,' Yeye alisema. 'Na wananaena hili lile, na lingine.') lakini mmemwamini Mungu, na kama mlivyomwamini Mungu, niaminini na Mimi."

Alikuwa Mungu aliayedhihirishwa, unaona. Aminini pia... "Nyumbani mwa Baba Yangu kuna mengi... au katika uchumi wa Baba Yangu, katika mipango ya Baba Yangu kuna ikulu nyingi. Naenda kuwaandalia mahali." Angalia jinsi yalivyo marefu—maili 1500 mraba. "Aisee, yako wapi?" Amekwenda kuyaandaa. Yeye ni Muumba. Huumba dhahabu yote hiyo. Barabara Zake zinaona kama kioo. Yeye ni Muumba. Anatengeneza makao.

Katika Ufunuo 21, alisema, "Nami, Yohana, niliona Mji ule Mtakatifu, Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu." Hapakuwa na bahari tena. Mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita.

Mbingu ya kwanza ilikuwa nini? Ilikuwa ule Utawala wa Miaka Elfu. Nchi ya kwanza ilikuwa nini?—ilikuwa hii. Itafanywa upya. Kama tu ilivyobatizwa na Nuhu katika siku za kuhubiri kwake; ilitakaswa na Kristo alipoinyunyizia Damu Yake, na kufanywa upya (kuondoa wadudu wote wabaya na kila kitu juu yake) katika kuifanya upya hapo mwishoni kwa ubatizo wa moto ambao utaua kila mdudu mbaya, kila maradhi, kila ugonjwa, kila uchafu uliowahi kuwa duniani. Dunia itapasuka, na kuwa dunia mpya. "Na naliona mbingu mpya na nchi mpya. Mbingu za kwanza na nchi za kwanza zimekwisha pita, na hapakuwa na bahari tena. Nami, Yohana, nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu."

Huko Mungu atakuwa na sifa Zake za kweli; wana wa kiume na wa kike, ambako atakuwa na ushirika nao katika utakatifu macho yao yakiwa yametiwa upofu yasmine dhambi yo yote. Hapatakuwa na dhambi tangu wakati huo na kuendelea. Hebu tukazane. Usidanganywe katika siku hii, lakini jitahidi kuingia mlangoni; kwani wote watakaoachwa nje, watakuwa wazinzi,

wenye tamaa mbaya. "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye." Wote pamoja—huko nje watakuweko wanawake wenye sifa mbaya, mwanaume mwenye sifa mbaya, na kadhalika, na ni wale tu waliokombolewa, na walio katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo wataingia mlangoni. Kwa hiyo jitahidini, marafiki; msidanganywe katika siku hii ya mwisho.

Huu ni wakati mkuu. Kila mtu ana hela. Kila mtu anaweza kufanya hili, na kila mtu anaweza kufanya lile. Kuna hela zinazomiminika kila upande na magari makubwa, na kila kitu; hapatakuwa na hata moja katika mji ule. Hapatakuwa na gari hata moja, ndege moja. La, utakuwa ustaarabu tofauti kabisa. Utakuwa tena ustaarabu, si wa ujuzi, si wa sayansi; bali wa kutojua dhambi, na imani katika Mungu aliye hai.

Hebu na tujitahidi kuingia katika huo, kwani hilo ndilo kusudi langu lote, ni kuingia katika Mji ule siku moja. Na angalia nyuma tu, njoo pamoja nami, uone kila mmoja wenu akipiga hatua taratibu, tutakapoimba, "Watakatifu wakiingia taratibu. Nataka kuwa katika hesabu ile, watakatifu watakapokuwa wakiingia taratibu." Na tuombe.

Baba mpenzi wa Mbinguni, siku zinapokaribia kwisha, na twaona hilo linakaribia, ile ahadi inakaribia. Tunaomba, Mungu mpenzi, kwamba utaweka hilo miyoni mwetu, ili tusikosee.

Mungu mpenzi, weka dhamiri zetu ziwe safi. Ifunike mioyo yetu, Bwana, macho yetu yafunikwe yasione mambo ya ulimwengu, na mambo yasiyo na maana ya ulimwengu—utukufu usio na maana wa kufanya mtu mkubwa fulani. Haidhuru ni wakubwa kiasi gani, wafalme wote, wenye mamlaka, wenye nguvu, na kila kitu kingine lazima kiangamie, nao hawatafufuka katika ufufuo wa kwanza; kwani imeandikwa, "Heri na mtakatifu ni ye ye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza ambapo juu ya hao mauti ya pili haina nguvu." Ee, Mungu, mauti ya pili, kifo cha roho, hakina nguvu. Amekombolewa.

Ee, Mungu, kuwazia kwamba moja ya saa hizi, mmoja ataenda kumzulu mwingine na atanyakuliwa. "Wawili kitandani, nitamchukua mmoja, na kumwacha mmoja. Wawili kondeni, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja."

Ee, Mungu, tusaidie kuwa safi mbele Zako, Bwana, haidhuru mwanadamu atafikiria nini juu yetu; kile watu wengine husema, Bwana, hebu utakatifu wetu...mazungumzo yetu yawe matakatifu. Hebu yakolee Neno la Mungu. Yakolee sana, Bwana, hata halitaonekana waa ndani yetu. Wakati tunaposihi katika makosa yetu yote kwamba Damu ya Yesu Kristo itasimama kati yetu na Mungu. Kwamba atatuangalia kupitia Damu ya Yesu. Si juu ya haki yetu, au eti sisi ni akina nani, au tulilotenda, bali katika fadhili Zake pekee. Mungu, tujalie hilo.

Hebu na yule ambaye ameketi hapa usiku wa leo na kusikia Ujumbe; hebu hata mmoja wao asipotee tangu mtoto mdogo hata aliye mzee kuliko wote. Hebu tamaa yao takatifu iwe kwa Mungu tu na Neno Lake. Hatujui ni wakati gani atatokea au ni saa gani awezayo kutuita juu huko kwenye hukumu. Hatujui ni saa gani atatuita, kama ilivyokuwa, kuchukua kadi yetu kutoka kwenye chombo cha kadi, kasema, "Ni saa ya kurudi nyumbani. Yakubidi kwenda." Mungu tusaidie kuwa safi. Tujalie hilo, Bwana.

Hebu tuishi mpaka kuja Kwake Bwana kama ikiwezekana. Hebu na tutende kila kitu kilicho katika uwezo wetu kwa upendo, na uelewano—kuelewa kwamba Mungu anauchunguza ulimwengu, siku hii ya leo, kutafuta kila kondoo aliyepotea. Hebu tuzungumze nao kwa maombi ya upendo yaliyokolea chumvi na Neno la Mungu, ili tuweze kumpata huyo wa mwisho kusudi tupate kwenda nyumbani, na tutoke katika Edeni hii ya kale ya Shetani hapa, Bwana, ambayo yote imejengwa juu ya tamaa mbaya, na wanawake wanaojiita warembo ulimwenguni kwa matangazo yao huko: "Tunatangaza, twataka wavulana waje wakiwa na jemu kwenye nyuso zao, na wasichana warembo wavae kaptura."

Moja kwa moja katika redio yetu na televisheni, na kila aina ya uchafu na unajisi na Hollywood; kila aina ya mavazi ya wanawake ya kinajisi, machafu, na takataka. Na wanaume wakiwa wamepotoka na wakivaa mavazi ya wanawake, na kukata nywele zao kama wanawake, na wanawake kama mwanamumee.

Ee, Mungu, ni saa ya kutisha jinsi gani tunayoishi. Loo, njoo, Bwana Yesu, njoo. Njoo, Bwana, tutakase kwa Damu. Ondoa takataka zote na hila kwetu. Tupe kuishi, Bwana. Hebu na tuishi chini ya Damu kila wakati mbele Zako. Ni hamu ya miyo yetu, na sala yetu ya kweli.

Ee Mungu, juu ya dawati hili, usiku wa leo, ambapo Injili imewekwa, Bwana Aliye Hai, hapa pana vitambaa na vifurushi vidogo ambavyo vinakwenda kwa wagonjwa na wanaoteseka. Hebu sala ya imani, Bwana, ianguke toka miyoni mwetu sasa mbele Zako. Basi, Bwana, kama kuna jambo lo lote lisilo safi ndani yetu, Bwana, chukua yetu... tupeleke hukumuni, sasa; na twaomba rehema.

Tufunulie tunalotenda vibaya, Bwana, ili tupate kuomba na kuchukua ile Damu na kujitakasa. Waponye watu hawa wagonjwa, na uwape afya, Baba. Ko kote inakoelekeea; ko kote waendako. Na iwe hivyo, Baba.

Tupe uthabiti kukutumikia, na Wewe pekee. Tujalie, Bwana. Wakirimie usalama watu hawa wapenzi ambaa wamo barabarani wakielekeea nyumbani. Asante kwa jinsi uliviyowaponya watu, na Dada Shepherd, na mvulana

mdogo wa Ndungu Shepherd aliyepata ajali ya baisikeli, ninaomba kwamba uovu wo wote usimfikie. Kijana huyo mdogo akiendesha baiskeli yake, naomba kwamba atakuwa mzima. Tunakushukuru kwa kuwaponya wengine ambao tumewaoombea. Nasi twajua kwamba kile tuombacho, tunapokea, kwa sababu tuna matumaini katika Yeye aliyetoa ile ahadi. Tupe neema Yako, Bwana, na tusamehe dhambi zetu, twaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Je! mnampenda? Mnamwamini? Mnajisikia vibaya na mmechoshwa na ufalme wa Shetani? Mnaamini ule Utawala wa Miaka Elfu unakaribia—ule Utawala Wake wa Miaka Elfu? Yake, hata kufikia Edeni Yake? Unaamini inatengenezwa hivi leo? Angalia, kila kitu kimewekewa msingi kwenye ujuzi wa akili. Kila kitu—kila kitu sharti kihakikishwe kisayansi kabla ya wao kukiamini, na huwezi kumhakikisha Mungu kisayansi. Yakubidi umkubali kwa imani, “kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.”

Ee, Mungu, sitaki nijue cho chote ila Damu ya Yesu Kristo ambayo hunisafisha na dhambi. Sijui cho chote, bali Yesu Kristo. Ni kama Paulo wa kale alivyosema, ndivyo nisemavyo pia, usiku wa leo, “Sijui neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa.”

Ni hilo tu nijualo kuwaambia, kwamba Biblia hii naamini kwa moyo wangu wote, kama najua moyo wangu, kuwa Neno kamilifu la Mungu lisiloghoshiwa. Kwa hili ninaishi. Kwa hili ninasimama. Na kama ningalikuwa na maisha elfu moja, ningependa kutoa kila sehemu yake kwa Neno hili, kwani ni Neno la Yesu Kristo. Nami sijali kiasi gani wanaweza kujaribu kutokukubaliana nalo, vipi sayansi inajaribu kusema haliaminiki, na kadhalika, kwangu mimi ndicho kitu cha pekee duniani niwezacho kutumainia ni hili Neno. Yeye ni wangu. Ninampenda. Je! hamumpendi?

Kama kuna dhambi moyoni mwako; kama kuna kosa moyoni mwako; kama una neno lo lote, omba sasa, na muombe Mungu akusamehe. Niombeeni, nitawaombea. Mungu awabariki ndiyo sala yangu.

Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

Mnapendana? Yohana alisema, “Watoto wadogo, mpendane.” Pendaneni, kwani pendo hufunika wingi wa dhambi. Sasa, hebu tupeane mikono.

Mungu awe nayi daima.
Hata twonane huko juu . . .

Sasa, muwe wema mmoja kwa mwingine, uwe mwema kwa kila mtu. Mtendee jirani yako mema. Jiweke bila doa hadi Yesu ajapo.

Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima.

Unampenda? Hiyo ndiyo sala yangu. Niombeeni; nitawaombea. Yanipasa nirudi Tucson, sasa. Na naomba kwamba Mungu atawabariki nyote. Toka hapo ninakwenda Canada, na kurudi Colorado, na kwenda huku na huko, huko na huko, na huko na huko, unaona. Mpaka... Ndugu Tony yuko huko, na jambo kubwa limetokea. Papo hapo chini ya Vatican huko Rumi, wanaita mukutano wa uufuo—niende huko na kufanya uufuo huko Rumi—huko Rumi. Ndio tu arudi. Watu wamekusanyika pamoja. Wana uwanja mkubwa wa michezo huko; huchukua maelfu ya maelfu, na wanantaka mimi kwenda kufanya uufuo. Wanataka kuona utukufu wa Mungu katika huduma. Sijui. Itanibidi niombe juu yake, na kuona ambalo Bwana ataniambia. Loo, jamani. Kumbukeni, ombeni, sote pamoja...

Tunatazamia kule kuja,
Kwa Mwokozi wetu mbarikiwa,
Loo, na angalia majani ya mtini
Sasa yakiwa kijani,
Injili ya ufalme Wake,
Imekwenda kwa kila taifa,
Na ni dhahiri tumekaribia mwisho.

Na kwa furaha hebu tupige mbiu ya ujumbe,
Wa kufunuliwa Kwake kubarikiwa.
Yuaja katika Utukufu, kila mtu na ajulishwe.
Basi amkeni enyi watakatifu wa Bwana,
Kwani mlale wakati mwisho unakaribia,
Hebu na tuwe tayari kwa mwito ule wa
mwisho.

Atageuka huko magharibi, na kurudi tena mojawapo ya siku hizi. Kumbukeni tu. Hakika atafanya hayo. Na hilo ni kweli. Mpaka wakati huo...

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, na tamu,
Ni jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
Nimejiinamisha;
Ndiye mfalme wa wafalme,
Kakika ya maisha,

Thamani, na tamu,
 Ni jina Lake Yesu;
 Thamani, na tamu,
 Ni jina Lake Yesu,

Sasa, katika mstari huu wa mwisho, hebu na tuuimbe na miyo iliyoinamishwa; “Peleka Jina la Yesu, liwe silaha zako. Utakapojaribiwa (mambo haya ya ufalme wa Shetani unaona,) lilia tu jina hilo,” hilo tu, kisha nenda zako. Linatenda kazi. Nimejaribu hilo. Hebu liamini tu, sasa, kwa sababu litafanya kazi, lilia Jina Lake takatifu katika maombi.

Peleka Jina la Yesu,
 Liwe silaha zako;
 Utakapojaribiwa, (Ndipo utafanya nini?)
 Lilia tu Jina hilo.
 (Utaji utafunika uso wako wakati huo.)
 Thamani, (Thamani) na tamu,
 Ni Jina Lake Yesu;
 Thamani, na tamu,
 Ni Jina Lake Yesu.

Tuinamishe vichwa vyetu, sasa, wakati nikimuomba Ndugu Beeler nyuma huko kuja hapa kwenye jukwaa.

[Ndugu Branham anaendelea kuimba—Mh.]

Tafadhali uturuhusu tupumukane, Ndugu Beeler, je, waweza kuturuhusu tupumukane kwa maombi?

Sasa, vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa na miyo yetu imeinamishwa. Ndugu Beeler, mmoja wa washiriki wetu hapa, Ndugu Estle Beeler, ndugu mzuri Mkristo, mtu mwaminifu. Nitamuuliza kama atawaruhusu watu waondoke, usiku wa leo, kwa maombi. Mungu akubariki, Ndugu Beeler.



EDENI YA SHETANI SWA65-0829
(Satan's Eden)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Agosti 29, 1965, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org